Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Aprili

# TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.05 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz



HALIUZWI

## Bima ni Kinga, Bima ni Ngao, Bima ni Maendeleo

Wasiliana nasi coi@tira.go.tz | Au tupigie +255 222 132 537 | FB, IG, X: //@tira_tz

# Yaliyomo

01



03




**Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

**Mhariri**
Hadija Maulid

**Waandishi**
Tabia Mchakama
Anna Massao

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba

01 Viongozi kutoka Eswatini Wazuru TIRA Kupata Uzoefu wa Masuala ya Kibima

03 Maafisa Mawasiliano Serikalini Wanolewa Utoaji wa Taarifa kwa Jamii na Maendeleo Sekta ya Mawasiliano

05 Elimu ya TAKAFUL yatolewa kwa wanafunzi wa MUM

06 Wanawake TIRA Washiriki Mkutano TAWiFA, Fursa Sekta ya Bima Zaelezwa

08 TIRA Yashiriki Mahafali ya 41 Kidato cha Sita Sekondari ya Jangwani, Elimu ya Bima Yatolewa; Kuendeleza Ushirikiano

10 Utoaji elimu ya bima; TIRA Yashiriki Maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa

11 TIRA: Tunaboresha Usalama Vyombo vya Moto Tupo Bega kwa Bega na Jeshi la Polisi Kuongeza Ufanisi

12 "Wasanii Kateni Bima kwa Ajili ya Kinga ya Afya Zenu na Bidhaa Zenu" – Mhe. Kabudi

14 TIRA Kanda ya Kati na Mikakati Kuimarisha Sekta ya Bima

17 Majibu ya Maswali yako kuhusu Bima

TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRAUpdates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Aprili 2025.




Scan
Kusoma Kidijiti

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
**info@tira.go.tz**

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
**www.tira.go.tz**

# Viongozi kutoka Eswatini Wazuru TIRA Kupata Uzoefu wa Masuala ya Kibima




Aprili 8, 2025 ujumbe wa watu 12 kutoka Eswatini ulioongozwa na Naibu Spika wa Bunge la nchi hiyo Mhe. Madala Mhlanga ulizuru ofisi ndogo za makao makuu ya TIRA Dar es salaam kwa lengo la kupata uzoefu wa maswala mbambali ya kibima yakiwemo yahusuyo Usimamizi wa Soko na maswala ya Sheria.

Baadhi ya wageni hao pia walitoka katika Bunge la nchi hiyo, Wizara ya Fedha na Mamlaka ya masuala ya huduma za Fedha zisizo za kibenki nchini humo (Financial Services Regulatory Authority), ambapo waliungana na wataalamu wengine kutoka TIRA na kufanya kikao kilichokuwa na lengo la kupeana uzoefu wa namna ya usimamizi na udhibiti katika soko la bima kwa pande zote mbili.

Aidha, kikao hicho kiliongozwa na Mkurugenzi wa Usimamizi kutoka Mamlaka Bw. Christopher Mapunda kwa niaba ya Kamishna wa Bima Tanzania ambapo wageni hao walipitishwa katika mada iliyoelezea hali ya soko la bima nchini ikijumuisha usimamizi wa soko la bima, sheria zinazotumika kusimamia soko la bima, Mamlaka ya Kamishna kwenye kusimamia soko la bima na mifumo ya TEHAMA.

Vilevile kulikuwa na mjadala uliojikita kwenye vipaumbele mbalimbali vya Mamlaka vikiwemo Utekelezwaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (UHI) na Uanzishwaji wa konsotia ya bima ya kilimo (TAIC). Awali Naibu Spika wa Nchi hiyo Mhe. Madala alieleza wapo katika mchakato wa uboreshaji wa sheria ya nchini humo na hivyo waliichagua Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi za Afrika zinazofanya vizuri katika masuala ya bima ili kuweza kujifunza.

Zaidi aliishukuru Mamlaka kwa elimu na uzoefu waliopata huku akiahidi kuendeleza ushirikiano kwa siku zijazo.




TIRA FOR SAFE
INSURANCE MARKET







# Maafisa Mawasiliano Serikalini Wanolewa Utoaji wa Taarifa kwa Jamii na Maendeleo Sekta ya Mawasiliano




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Maafisa Uhusiano na Mawasiliano Serikalini (TAGCO) 2025 uliofanyika mkoani Morogoro, ambapo uliwakutanisha Maafisa Mawasiliano wa Serikali kwa lengo la kubadilishana mawazo na kujadili masuala mbalimbali ya mawasiliano Serikalini.

Mkutano huu wa siku tano ulianza April 8 – 12 2025, ukiwa umejikita katika kujadili mafanikio, mikakati na changamoto ya taaluma, kujifunza, kuimarisha ujuzi, kuandaa mikakati endelevu ya maendeleo ya tasnia, pamoja na kuibua mbinu mpya zitakazochochea ubunifu katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali ndani ya sekta ya mawasiliano.

TIRA ilishiriki mkutano huo ambapo maafisa mawasiliano walishiriki na kuweza kuongeza ujuzi zaidi kupitia mada mbalimbali zilizowasilishwa zikiwemo namna ya kushirikisha shughuli za mawasiliano na Dira ya Taifa ya Maendeleo, namna ya utoaji taarifa wakati wa majanga, matumizi ya mitandao ya kijigitali Serikalini, mada zote ziliwasilishwa na wabobezi mbalimbali wa tasnia hiyo. Ujuzi huu utawasaidia kufikisha habari zenye tija na manufaa kwa wananchi.

Aidha, katika hotuba ya Mwenyekiti wa TAGCO Bw. Karim Meshack alitoa rai kwa maafisa mawasiliano kufanya kazi kwa weledi, ushirikiano na ubunifu lakini pia kuhakikisha wanatoa habari sahihi na kwa wakati sahihi kwa jamii katika kutangaza maendeleo mbalimbali yanayofanywa na Serikali.

Fursa hiyo mahsusi iliwapa wanataaluma wa mawasiliano kukumbushana umuhimu wa kushirikiana, kufanya kazi kwa weledi na kujituma, huku wakihakikisha kila mmoja anatoa mchango chanya katika kuiboresha sekta ya mawasiliano serikalini.







# Elimu ya TAKAFUL yatolewa kwa wanafunzi wa MUM




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilitoa elimu ya Takaful kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro (MUM) ikiwa ni utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kutoa elimu ya bima kwa umma kupitia makundi tofauti ya jamii, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii.

Elimu ya Takaful kwa wanafunzi hao ilitolewa tarehe 10 Aprili 2025 katika ofisi ndogo ya Makao Makuu ya TIRA jijini Dar es salaam na wataalam wabobezi masuala ya bima ambao ni Bw. Paul Ngangaji na Bi. Raya Abdallah ambao walieleza sekta ya bima nchini imekata kiu ya Watanzania wengi ambao walikuwa hawakati bima kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo imani ya kutotaka riba.

Takaful ni mfumo wa bima wa ushirikiano unaozingatia misingi ya Shariah, ambapo wanachama huchangia fedha kwa pamoja ili kusaidiana katika kukabiliana na hasara au majanga yanayoweza kutokea.

Akitoa shukrani zake za dhati mwalimu aliyeambatana na msafara huo aliishukuru Mamlaka na kueleza kuwa wanafunzi hao wamepata kitu chema na ambacho hakitatoka kwenye vichwa vyao na elimu hiyo itawasaidia kuwa mabolozi wema wa bima kwa jamii inayowazunguka.



# Wanawake TIRA Washiriki Mkutano TAWiFA, Fursa Sekta ya Bima Zaelezwa




Wanawake TIRA walijumuika na Wanawake wengine kutoka sekta ya Fedha Tanzania Aprili 16 2025 Dodoma kushiriki Mkutano Mkuu wa Mwaka ulioandaliwa na jumuiya ya wanawake katika sekta ya fedha (TAWiFA) ambapo Dkt. Doto Biteko Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, alikuwa Mgeni Rasmi.

Wakati wa hotuba yake Mhe. Biteko alisisitiza juu ya elimu ya fedha kwa wanawake wa vijijini ili waepukane na mikopo umiza inayosababisha kuchukuliwa baadhi ya mali zao za ndani wanaposhindwa kurejesha mikopo hiyo.

Kwa upande wake Naibu Kamishna wa Bima Tanzania, Bi. Khadija Issa Said alieleza namna sekta ya bima inavyozidi kukua hapa nchini, huku wanawake katika sekta hiyo wakitoa mchango katika matumizi ya bidhaa za bima, lakini pia mchango kupitia uongozi katika sekta hiyo.

Bi. Khadija aliwataka wanawake kwenye sekta ya fedha kuendelea kujibiidisha kazini na kushirikiana ili waendelee kukuza sekta hiyo.

Aidha Bi. Fikira Mtomola, Rais wa TAWiFA alisema mkutano huo uliokuwa na kauli mbiu ya "Wekeza kwa wanawake ili kuchochea maendeleo" una engo la kuongeza uelewa na uwajibikaji wa wanawake katika sekta ya fedha nchini na kutengeneza mazingira wezeshi kwa wanawake ili kujumuishwa na kuongoza katika mambo mbalimbali ya kifedha.

Mkutano huo ulitanguliwa na matukio mbalimbali ambapo tarehe 11 Aprili 2025 kulikuwa na zoezi la upandaji wa miti ya matunda zaidi ya 2000 katika shule za msingi za mkoa huo na tarehe 12 Aprili 2025 kulikuwa na mkutano wa utoaji elimu ya fedha kwa wanawake wajasiriamali uliofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Zabibu, Dodoma.








TAWiFA

# TIRA Yashiriki Mahafali ya 41 Kidato cha Sita Sekondari ya Jangwani, Elimu ya Bima Yatolewa; Kuendeleza Ushirikiano



Katikati ya jiji la Dar es Salaam eneo la Jangwani karibu na soko maarufu la Kariakoo inapatikana moja kati ya shule kongwe Tanzania iliyoanzishwa Mei 28, 1928, Shule ya Sekondari ya wasichana Jangwani. Aprili 24, 2025 yalifanyika mahafali ya 41 ya kidato cha sita ambapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilipata heshima ya kushiriki kama Mgeni Rasmi.

Aidha, wakati wa hotuba yake Mgeni Rasmi, Meneja wa TIRA Kanda ya Mashariki Bw. Zakaria Muyengi kwa niaba ya Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware aliupongeza uongozi wa shule hiyo pamoja na wanafunzi kwa ufaulu mzuri katika mitihani ya kitaifa kwa miaka mbalimbali na kuahidi Mamlaka kuendeleza ushirikiano nao ambapo TIRA na wadau wa Bima watatoa msaada wa samani mbalimbali zikiwemo meza na viti kulingana na upungufu uliopo, lakini pia Mamlaka itasaidia baadhi ya wanafunzi wenye changamoto za ulemavu kupata bima za afya na pia







kutoa mchango wa ujenzi wa jengo la kulia chakula, ikiwa ni changamoto zilizoainishwa.

Mamlaka pia ilitoa ujumbe kwa walimu, wazazi na wanafunzi kutumia bidhaa mbalimbali za bima ikiwemo bima ya maisha na bima za kawaida ili kuweza kujikinga na majanga yasiyotarajiwa, lakini pia walikaribishwa Ofisi za Mamlaka hiyo kupata semina zaidi kuhusu masuala ya bima.

Naye, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Bi. Bhoke Nyagonde aliishukuru TIRA kwa ushirikiano walioonesha na msaada uliotolewa na kusisitiza lengo lao kubwa ni kuongeza uzalendo na kutoa elimu bora ili kujenga wasichana wazalendo kwa taifa lao na kuwa viongozi bora wa badae. Moja ya mikakati ya Mamlaka ni kuhakikisha elimu ya bima inaanzia kwa watoto na vijana kama taifa la kesho na hivyo wakati wote hufanya semina na mikutano mbalimbali kwa wanafunzi na wanachuo ili kuhakikisha elimu ya bima inamfikia kila mmoja huku ikiendeleza ushirikiano katika kukuza sekta ya elimu nchini.

# Utoaji elimu ya bima; TIRA Yashiriki Maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania iliungana na taasisi mbalimbali kushiriki Maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa kama jukwaa la kutoa elimu ya bima kwa wananchi mbalimbali waliotembelea mabanda ya maonesho, lengo kubwa ikiwa ni kufikisha elimu ya bima kwa wananchi.

Maonesho hayo yalianza tarehe 24 Aprili, 2025 na yalimalizika Aprili 30, 2025 katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Wakati wa ufunguzi wa Maonesho hayo yaliyoandaliwa na Mfuko wa Utamaduni Tanzania, Mgeni Rasmi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Metheusula Ntonda alizipongeza Taasisi zilizoshiriki katika kuendeleza kazi za Utamaduni na Sanaa lakini pia Mhe. Ntonda alielezwa shughuli mbalimbali za Mamlaka alipotembelea banda la Mamlaka hiyo, zikiwemo kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima, kuandaa na kutoa kanuni na miongozo mbalimbali inayosimamia soko la bima, kutoa elimu ya bima kwa umma, kulinda haki za mteja wa bima lakini pia kuishauri Serikali juu ya masuala ya bima, na kuipongeza Mamlaka kwa kazi nzuri ya uelimishaji.

# TIRA: Tunaboresha Usalama Vyombo vya Moto Tupo Bega kwa Bega na Jeshi la Polisi Kuongeza Ufanisi




Meneja wa TIRA Kanda ya Mashariki  Bw. Zakaria Muyengi alieleza kazi za kanda hiyo inayohudumu mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro wakati wa ugeni wa Jeshi la polisi uliotembelea banda la TIRA na uliongozwa na Mkaguzi Msaidizi Masjala ya Polisi Afande RPS Bi. Rose Tittey wa Mkoa wa Kipolisi wa Ilala.

Aidha katika mazungumzo yao, walikubaliana na kupanga kuboresha mahusiano kati ya TIRA na mkoa wa kipolisi Ilala katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na bima hasa uhalifu kwenye bima za vyombo vya moto, lakini pia walijadilina kuhusu utoaji elimu ya bima kwa jeshi la polisi na kushirikishana fursa zilizopo katika soko la bima kama saccos ya jeshi la polisi kuitumia fursa ya kufanya shughuli  za uwakala wa bima.

Jeshi la polisi Tanzania ni moja kati ya wadau wakubwa wa Mamlaka kwa sababu ya ushirikiano uliopo katika kazi za ufatiliaji na tathimini hasa wa bima za vyombo vya moto kama gari na pikipiki.

# “Wasanii Kateni Bima kwa Ajili ya Kinga ya Afya Zenu na Bidhaa Zenu” – Mhe. Kabudi




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Palamagamba Kabudi aliyasema hayo katika hotuba yake wakati wa kufunga rasmi Maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa, na aliwasisitiza wasanii hapa nchini kuhakikisha wanakata bima za afya na nyinginezo kwa ajili ya kuzilinda kazi zao.

Mhe. Waziri aliyafunga rasmi maonesho hayo tarehe 30 Aprili ambayo yalianza rasmi Aprili 24, 2025, katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Awali alipotembelea banda la TIRA katika maonesho hayo alipewa maelezo na Meneja wa TIRA kanda ya Mashariki Bw. Zakaria Muyengi kuhusu majukumu ya Mamlaka na vipaumbele vyake ikiwemo usimamizi na udhibiti wa bima ya afya kwa wote, ambapo Mamlaka inasimamia na kudhibiti skimu za bima ya afya kwa kuhakikisha zinatoa huduma za bima ya afya kwa wanachama wake na vituo vya huduma ya afya vilivyoingia mkataba na skimu kufanya kazi zake kwa weledi ikiwemo kukidhi kigezo cha usajili.

Aidha, Mhe. Kabudi pia alizipongeza taasisi za fedha zilizoshiriki ikiwemo TIRA kwa ushiriki wake na kuwatangaza kuwa wadau wa kudumu wa Maonesho hayo ambayo yatafanyika tena mwaka 2026, Oktoba jijini Arusha.

Naye, Bi.Nyakaho Mturi Mahemba, Afisa Mtendaji Mkuu kutoka Mfuko wa Utamaduni Tanzania ambao ndio waandaaji Maonesho hayo aliwasisitiza wasanii hasa vijana kuchangamkia fursa zilizopo katika maonesho hayo kutoka katika taasisi za Serikali na binafsi kupitia bima, uwekezaji na nyinginezo ili waweze kunufaika katika kazi zao.



# Ana kwa Ana

na Hadija Maulid

# TIRA Kanda ya Kati na Mikakati Kuimarisha Sekta ya Bima

**Mpendwa Msomaji wetu wa TIRA Upadates, karibu katika ukurasa huu unaokuleta maswala mbalimbali yanayojiri katika sekta ya bima ukikutanisha na wadau mbalimbali wakielezea yanayojiri katika maeneo yao ya utendaji.**

**Na toleo hili linakukutanisha na Meneja TIRA Kanda ya Kati yenye ofisi zake jijini Dodoma.**

**Karibu!**



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inaendelea kukuza uelewa na utekelezaji wa sheria za bima katika mikoa ya Dodoma, Iringa na Manyara kupitia Ofisi ya Kanda ya Kati, inayoongozwa na Bw. Frank Fred Shangali.

Katika mahojiano na Meneja Mahusiano na Mawasiliano kwa Umma, Bi. Hadija Maulid, Bw. Shangali anaeleza kuhusu utekelezaji wa majukumu yote ya msingi kuanzia utafiti wa soko, utoaji elimu kwa umma, usajili na utoaji wa leseni, ukaguzi na utekelezaji wa sheria ili kuhakikisha huduma za bima zinawafikia wananchi kikamilifu na kwa viwango vinavyokubalika.

Bw. Shangali anaeleza kuwa Kupitia kampeni za redio, televisheni, mitandao ya kijamii na mikutano ya hadhara, TIRA hutoa elimu kuhusu faida za bima kwa wananchi na taasisi za serikali, huku ikiwapa watoa huduma miongozo ya kuendesha biashara za bima kwa kufuata kanuni, sheria na utaratibu za uendeshaji wa sekta ya bima nchini.

Kanda hii imesajili zaidi ya matawi ishirini (20) ya makampuni ya bima na benki ishirini na tatu zinazotoa huduma za benki wakala wa bima 'bancassurance', sambamba na kusimamia mawakala wa bima.

Aidha, anaendelea kutanabahisha kuwa Kupitia wataalamu kwenye ofisi ya Kanda ya Kati Mamlaka inafanya kaguzi mara kwa mara magari barabarani, vituo vya afya, vituo vya mafuta na mali nyingine zilizo chini ya bima za lazima. Mwaka huu pekee, imekagua zaidi ya vituo thelathini vya mafuta mkoani Iringa na kutoa maelekezo kwa watoa huduma waliokiuka taratibu.

Akizungumzia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Bw. Shangali alisema Kwa sasa ofisi ya Kanda ya kati imepokea maombi ya hospitali 107 ambazo ni hospitali za serikali na



binafsi zinazohudumiwa na mifuko ya Bima ambapo kwa mujibu wa Muongozo uliotolewa na Mamlaka hospitali zote zinazohumdumia wateja wao kupitia mifuko ya Bima wanapaswa kupata Ithibati kupitia Mamalaka ya usimamizi wa Bima.

Katika eneo la ulinzi wa mlaji, TIRA inatekeleza kanuni za amana zinazotaka kakampuni ziweke asilimia 50 ya mtaji kwenye benki kuu ya Tanzania na kiasi kingine kiwekwe kwenye benki za kibiashara kama amana (FDR) ya fidia endapo kampuni itashindwa kujiendesha.

Ofisi ya kanda pia hushughulikia malalamiko yote ya wateja wanaotumia huduma za bima kupitia dirisha la huduma kwa wateja, barua-pepe na namba ya simu ya bure ama ana kwa ana wanapotembelea ofisi za kanda hiyo.

Ingawa bado kuna changamoto kama vile uelewa mdogo wa masuala ya bima miongoni mwa wananchi mbalimbali wale wanaotumia na wasiotumia huduma za bima, Mamlaka imeedelea kutoa elimu kimkakati ili kuwafikia wote. Licha ya changamoto hiyo, Ofisi ya Kanda ya Kati ya TIRA imeendelea kupaza sauti kuhusu fursa ambazo sekta ya bima inayo kwa watanzania hususan katika kukuza na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi pamoja na miradi mikubwa ya kimkakati kama reli ya SGR, inayohitaji bima maalumu.

Amesisitiza kuwa mikoa ya Dodoma, Iringa na Manyara ina fursa tele za kiuchumi katika madini, kilimo, ufugaji na biashara, na kwamba bima ndiyo “uhakika, usalama na nafuu” kwa wawekezaji wanaotaka kulinda mitaji na kukuza maendeleo endelevu.

Kwa jumla, dhamira ya TIRA ni kuifanya bima iwe sehemu ya utamaduni wa Mtanzania kwa kutoa elimu wazi, kusimamia kampuni kwa karibu na kulinda haki za wateja, hivyo kuweka msingi thabiti wa ustawi wa kiuchumi ndani ya kanda na kote nchini.



# Majibu ya Maswali yako Kuhusu Bima

*Pata majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara*



## Bima ni nini?

Bima ni mkataba wa kisheria kati ya pande mbili yaani kampuni ya bima na mtu binafsi, kikundi au kampuni (mbima), ambapo kampuni ya bima inaahidi kulipa fidia iwapo janga lililokatiwa bima litatokea na kusababisha hasara. Hivyo, bima ni nia ya kuhamishia majanga kwa kampuni za bima na kupata kinga dhidi ya majanga mbalimbali yasiyotarajiwa. Bima hukatwa kwa ajili ya kukinga majanga mbalimbali yanayotuzunguka kila siku.

## Majanga ni nini?

Ni hatari yeyote isiyotabirika inayoweza kusababisha upotevu wa fedha, maisha na mali. Hatari hizi zinaweza kutokea katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kila siku. Hivyo, matukio kama ajali za vyombo vya usafiri, moto, mafuriko, magonjwa, ukame ni baadhi tu ya majanga yanayoweza kumkumba mwananchi.

## Bima ina umuhimu gani kwa mali na maisha ya mwananchi?

Bima ni muhimu kwani inahakikisha usalama wa kukabiliana na aina yoyote ya changamoto maishani. Bima ni sehemu muhimu sana katika mipango ya mwananchi katika uwekezaji wa kiuchumi na kijamii.

## Je, ni nani anastahili kuwa na Bima?

Bima ni nyenzo muhimu sana kwa kila mwananchi, hivyo hakuna anayebaguliwa ama kupewa kipaumbele sana katika kupata huduma za bima.

Hii ni kwa sababu kila mmoja kwa wakati fulani hukumbwa na janga aidha la kiuchumi (kupata hasara katika Biashara, kilimo, ufugaji n.k) na kijamii (yaani kuuguliwa, kufiwa na hata watoto kukosa ada na chakula n.k). Hivyo, kuzingatia aina hii ya uwezekano wa kupatwa majanga, jamii yote huhitaji bima za aina mbalimbali kulingana na uhitaji.

## Ni nani aliyepewa dhamana ya kutoa huduma za Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, Soko la Bima nchini linasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo hutoa leseni kwa kampuni za bima ambazo hubeba dhamana ya kutoa fidia kwa wananchi waliokata bima.

Pia, wananchi wanaweza kupata huduma za bima kupitia Washauri na Madalali wa Bima, Mawakala wa Bima kupitia Benki na Mawakala wa Bima waliosajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuna watoa huduma za bima wanaosajiliwa na Mamlaka kama Wakadiria Hasara, Wakaguzi Binafsi na Wakala wa Ufuatiliaji wa Fidia.

## Ni wakati gani Bima inahitajika?

Bima inahitajika mara tu unapokuwa hauna uhakika na uwezekano wa kuwa katika hali yako ya awali iwapo janga litakupata. Hivyo, ni vema ikafahamika kuwa bima hukatwa mapema ili kujikinga na janga kabla halijatokea. Iwapo itakatwa baada ya janga kutokea haitofaa kutoa fidia kwa janga lililopita.

## Je, ni lazima kuwa na Bima?

Kimsingi, mwananchi anawajibika kukinga mali na wapendwa wake kwa hiari yake kwa kuwakatia bima. Pamoja na hiari hiyo, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya Mwaka 1973, iliyorekebishwa 2002 imewapasa wamiliki wa vombo vya moto wanaotumia barabara za umma kukata bima ndogo (Third Party Insurance) ili kumkinga mtu wa tatu dhidi ya majanga yanayosababishwa na vyombo vya moto.

## Je, ni nani mnufaika wa Bima?

Bima hunufaisha wamiliki wa bima au wakata (policyholders) na wahanga kulingana na aina

ya bima iliyokatwa na majanga yaliyosababisha hasara. Kwa mfano, Bima za Maisha na Bima za Afya hunufaisha mkataji bima ama wanufaika walioandikwa katika mkataba wa bima.

Kwa upande wa Bima za Muda Mfupi, mnufaika wa kwanza huwa ni mkata bima hususan kwenye bima za moto, kilimo, ajali, biashara, n.k. Bima ndogo (Third Party) hunufaisha moja kwa moja mtu wa tatu aliyesababishiwa janga iwe kuumizwa yeye mwenyewe ama kuharibiwa mali zake.

## Mkata bima ana wajibu katika suala zima la kupata huduma za Bima?

Ni kweli kuwa mkata bima anao wajibu katika hatua za kukata bima na wakati bima iko hai.

Wakati wa kukata bima atawaibika kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa ukweli usiyo na shaka (bila kuongopa), kujaza fomu ya uhitaji wa bima na kutaja wanufaika (hii ni kwa Bima za Maisha na Bima za Afya), kuwa na nyaraka zote muhimu wakati wa ukataji bima kabla ya kuchukua mkataba wa bima; kufanya madai kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa bima na kufuata mchakato wa madai.

## Je, pindi mkata bima anapopatwa na janga, ni wapi anatakiwa kutoa taarifa?

Pindi janga lililokatiwa bima linapotokea mkata bima mwenye mkataba wa bima anapaswa kutoa taarifa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga dhidi ya mali yake ili kuwezesha hatua zingine za fidia kuendelea. Utaoaji wa taarifa uzingatie taratibu zilizowekwa katika mkataba wa bima. Inashauriwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 baada ya janga kutokea.

Mhanga anaweza pia kutoa taarifa kwa wakala au dalali wa bima aliyemkatia bima. Lakini isisahaulike kuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na ngazi mbalimbali za Serikali, kwa mfano: inapotokea ajali, mkata bima atoe taarifa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani au nyumba inapoungua ni vema kutoa taarifa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa upande mwingine kuna Ofisi za Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata.

Kutoa taarifa sehemu zote hizi hujenga msingi mzuri wa mkata bima kufidiwa bila mashaka ya tukio kwani linakuwa limehakikiwa na ngazi husika.

## Ni muda gani umewekwa kwa kampuni kushughulikia fidia kwa mhanga wa ajali au kuharibikiwa na mali iliyowekewa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, kampuni ya bima inapaswa kushughulikia madai ya wateja kwa muda mfupi kulingana na ukubwa wa janga na uthibitisho wa janga lenyewe kuwa halali. Baada ya kujiridhisha kuwa janga hilo ni sahihi na kutoa hati ya kukubali janga, kampuni itawajibika kutoa fidia kwa mteja ndani ya siku zisizozidi 45.

## Ni jinsi gani mteja anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ndicho chombo cha Serikali kinachowajibika kumlinda mteja wa bima (mkata bima). Hivyo, ni sahihi kabisa

kwa mnufaika wa huduma za bima kuleta lalamiko lake dhidi ya huduma za bima anazopewa na kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa TIRA kupitia barua pepe au simu, kutegemea uko eneo gani nchini. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko kupitia tovuti: www.tira.go.tz ambapo utajaza fomu ya malalamiko na kuiwasilisha.

## Je, kuna tofauti kati malalamiko ya Bima na migogoro ya Bima?

Malalamiko ya bima ni tofauti kigodo na migogoro ya bima, kwani malalaiko ya bima hutokana na huduma hafifu zinazotolewa na watoa huduma wa bima kwa wananchi waliosajiliwa na Mamlaka na mara nyingi aina hii ya malalamiko uhusisha wahanga wa ajali (third party) na haya huwasilishwa kwa Kamishna wa Bima kwa hatua stahiki.

Migogoro ya bima ni ile inayohusisha mteja kutokubaliana na kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Migogoro hii hupelekwa kwenye Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) kwa hatua zaidi.

## Je, kuna Bima kwa ajili ya kilimo na mifugo?

Soko la Bima nchini linaendelea kukua kila siku. Aina mbalimbali za bima zinatolewa ikiwemo Bima za Kilimo naBima za Mifugo. Bima ya Kilimo hukatwa kwa ajili ya kukinga moto, mafuriko, ukame, wanyama na wadudu waharibifu. Kwa upande wa Bima ya Mifugo, hutolewa kwa ajili ya kukinga magonjwa, upotevu na vifo.

## Je, TIRA ina mifumo yoyote ambayo inaitumia katika usimamizi wa shughuli za Bima kwenye soko?

Ndiyo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina mifumo mingi katika utoaji wa huduma za bima: Mafno: Mfumo wa TIRA-MIS unaotumika kukata bima na kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto na mali za mteja, mfumo mwingine ni Tanzania Import Insurance Portal (TIP) kwa ajili ya bima za mizigo kutoka nje ya nchi kwa njia meli (bahari) na dege (anga).

Pia mfumo wa Risk Based Supervision (RBS) kwa ajili ya upokeaji wa taarifa na uchambuzi wa viashiria vya majanga. Mifumo hii yote imeunganishwa na taasisi stahiki za Serikali pamoja na watoa huduma za bima.

## Je, ninaweza kuhakiki bima ya chombo cha moto na mali zangu?

Ndio, unaweza kuhakiki bima yako kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.

## Je, Kuna Bima kwa ajili watu wa kipato cha chini?

Ndio. Ipo bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini, bima hii hufahamika kama "'microinsurance'. Ni bima ndogo ambayo ni kwa ajili ya kumkinga mtu asiyeweza kuingia kwenye utaratibu wa bima yenye gharama kubwa kutokana na kiwango cha fedha anachokipata.

Mfano kwa wale wanaofanya shughuli za uAprilinga, mama/baba lishe, na wengine wenye biashara ndogo ndogo. Bima hizi hulipa fidia endapo mbima atapata hasara kwenye biashara yake aliyoikatia bima.

# Tupo nchi nzima!

## Makao Makuu Dodoma, Ofisi ya Zanzibar, Ofisi ya Dar es Salaam pamoja na Ofisi za Kanda

| Kanda | Mkoa |
|---|---|
| **Kanda ya Nyanda za Juu Kusini** | Mbeya, Njombe na Songwe |
| **Kanda ya Kaskazini** | Arusha, Kilimanjaro na Tanga |
| **Kanda ya Ziwa** | Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu na Geita |
| **Kanda ya Mashariki** | Dar es Salaam, Pwani na Morogoro |
| **Kanda ya Kati** | Dodoma, Manyara na Iringa |
| **Kanda ya Magharibi** | Tabora, Shinyanga na Singida |
| **Kanda ya Kusini** | Lindi, Mtwara na Ruvuma |
| **Kanda ya Ziwa Tanganyika** | Katavi, Rukwa na Kigoma |
| **Kanda ya Unguja** | Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Mjini Magharibi - Chakechake |
| **Kanda ya Pemba** | Kaskazini Pemba na Kusini Pemba - Wilaya ya Kati |

**TIRA - Kwa soko salama la Bima**



# TIRA & 2025

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

**FB, IG, X:** //@tira_tz
www.tira.go.tz